THE ACTION CHALLENGE

Mwongozo wa Kuwasilisha Picha na Video

Hifadhi kumbukumbu ya hatua yako. Shiriki hadithi yako. Heshimu jamii yako.

Kila hatua ina hadithi inayostahili kushirikiwa. Iwe unasafisha eneo la umma, unarahisisha watu wote kufika na kutumia mahali, unatengeneza kitu chenye manufaa, au unaifanya jamii yako kuwa salama zaidi, picha na video huwasaidia wengine kuona kinachowezekana.

Mwongozo huu unaeleza jinsi ya kuhifadhi kumbukumbu na kuwasilisha hatua yako ya kijamii huku ukilinda faragha, heshima na usalama wa watu.

Katika mwongozo huu

1. Nini cha kupiga picha
2. Mwongozo wa picha
3. Mwongozo wa video
4. Heshimu faragha, ridhaa na utu
5. Kuwa salama na mkweli
6. Ufikivu na kumbukumbu zinazomjumuisha kila mtu
7. Jinsi ya kuwasilisha picha na video zako
8. Jinsi Amplified Access inavyoweza kutumia picha na video zako
9. Jinsi tunavyolinda picha na video zilizowasilishwa
10. Orodha ya mwisho kabla ya kuwasilisha

Nini cha kupiga picha

Picha na video zako zinapaswa kutusaidia kuelewa mambo matatu:

KABLA

Tatizo

Onyesha tatizo au hali ambayo jamii yako ilitaka kuboresha.

WAKATI WA KAZI

Hatua

Onyesha ulichofanya wewe au jamii yako kushughulikia tatizo hilo.

BAADAYE

Matokeo

Onyesha kilichobadilika, kilichofanikiwa, au ulichojifunza.

Huhitaji vifaa vya kitaalamu. Simu janja inatosha.

Mwongozo wa picha

Fanya

- ✓ Piga picha zilizo wazi na zenye mwanga wa kutosha.
- ✓ Piga picha ya kazi halisi inayofanyika.
- ✓ Onyesha picha za kabla na baada pale inapowezekana.
- ✓ Tumia picha za kawaida na halisi.
- ✓ Piga picha watu wanaoweza kutambulika kwa ruhusa yao tu.
- ✓ Lenga hatua, jamii na matokeo.
- ✓ Piga picha kutoka pande tofauti, za karibu na za mbali.
- ✓ Piga picha za shughuli bila kuonyesha nyuso pale faragha au usalama unapohitaji hivyo.

Usifanye

- ✗ Usiigize shughuli au kujifanya kazi ilifanyika wakati haikufanyika.
- ✗ Usiwasilishe picha zilizotengenezwa na AI kama ushahidi wa shughuli halisi.
- ✗ Usitumie picha zilizochukuliwa kutoka mtandaoni au kutoka miradi ya watu wengine.
- ✗ Usipige picha watu wanaoweza kutambulika bila ruhusa yao.
- ✗ Usionyeshe watu katika hali ya aibu, ya kudhalilisha au ya hatari.
- ✗ Usiweke taarifa binafsi nyeti, kama vitambulisho, namba za simu au anwani za makazi.
- ✗ Usitumie vichujio au uhariri unaopotosha kilichotokea.

Mwongozo wa video

Fanya

- ✓ Rekodi video fupi, ikiwezekana sekunde 30–60.
- ✓ Shika simu yako bila kutikisika na hakikisha unachorekodi kinaonekana.
- ✓ Rekodi mahali patulivu mtu anapozungumza.
- ✓ Eleza tatizo, hatua iliyochukuliwa na matokeo.
- ✓ Zungumza kwa kawaida kwa lugha unayoimudu vizuri.
- ✓ Tumia maandishi kwenye video, lugha ya alama au njia nyingine za mawasiliano zinazofikika pale inapofaa.
- ✓ Onyesha shughuli halisi na ushiriki wa kweli wa jamii.
- ✓ Omba ruhusa kabla ya kurekodi watu wanaoweza kutambulika.

Usifanye

- ✗ Usirekodi video ndefu zisizo na lengo wazi.
- ✗ Usiweke muziki wa nyuma wenye sauti kubwa unaofanya maneno yasisikike vizuri.
- ✗ Usirekodi watu waliokataa kushiriki.
- ✗ Usirekodi shughuli za hatari wala kuwahimiza watu kujiweka hatarini kwa ajili ya kamera.
- ✗ Usiweke madai ya kupotosha wala kutia chumvi matokeo.
- ✗ Usirekodi mazungumzo ya faragha bila ruhusa.
- ✗ Usitumie video zilizotengenezwa na AI au zilizobadilishwa kama ushahidi wa hatua zilizokamilika.

Heshimu faragha, ridhaa na utu

Usalama, utu na maamuzi ya watu yanatangulia.

- Omba ruhusa kabla ya kupiga picha au kurekodi video ya watu wanaoweza kutambulika.
- Eleza kwa nini maudhui haya yanakusanywa, yanaweza kutumikaje, na nani anaweza kuyaona.
- Pata ruhusa inayofaa kutoka kwa mzazi au mlezi halali kabla ya kuwaonyesha watoto wanaoweza kutambulika, na heshimu matakwa ya mtoto.
- Epuka kuonyesha watoto au watu walio hatarini wanaoweza kutambulika pale ambapo ridhaa au usalama hauna uhakika.

- Mheshimu yeyote asiyetaka kuonekana kwenye picha au video.
- Epuka kufichua taarifa binafsi, anwani za makazi au maeneo nyeti.
- Wape watu nafasi ya kukataa kushiriki bila madhara yoyote kwao.
- Mtu akiondoa ruhusa yake, ijulishe timu ya Action Challenge mara moja.

MUHIMU

Kushiriki katika hatua ya kijamii hakumaanishi moja kwa moja kukubali kupigwa picha, kurekodiwa video, au kuonyeshwa hadharani.

Kuwasilisha maudhui si sawa na kutoa ruhusa ya kuyachapisha hadharani. Amplified Access itatofautisha kati ya ruhusa ya kuwasilisha kumbukumbu na ruhusa ya kushiriki hadharani maudhui yanayowatambulisha watu.

Kuwa salama na mkweli

- Usijiweke wewe wala wengine hatarini ili kupata picha au video.
- Usikatize huduma muhimu wala kusababisha hatari unaporekodi.
- Heshimu kanuni za jamii na pata ruhusa yoyote inayohitajika.
- Epuka kurekodi ugomvi, ajali au hali zinazoumiza watu.
- Usibuni matokeo, usitumie video za zamani kama ushahidi mpya, wala usipotoshe kuhusu nani alishiriki.
- Kama hatua bado inaendelea, eleza wazi kwamba bado inaendelea badala ya kuionyesha kama imekamilika.
- Usifichue taarifa zinazoweza kuwaweka washiriki katika hatari ya kunyanyaswa, kubaguliwa au kulipiziwa kisasi.

Lengo ni kuhifadhi kumbukumbu ya hatua yenye maana, si kutengeneza hadithi inayoonekana kamilifu.

Ufikivu na kumbukumbu zinazomjumuisha kila mtu

Kila mtu anapaswa kuweza kuhifadhi kumbukumbu ya hatua yake ya kijamii, bila kujali lugha, ulemavu au upatikanaji wa teknolojia.

- Wasilisha maelezo au simulizi kwa lugha unayoimudu vizuri zaidi.

- Tumia mawasiliano ya kuongea, kuandika au lugha ya alama pale inapofaa.
- Weka maandishi kwenye video au maelezo mafupi ya maandishi pale inapowezekana.
- Toa kumbukumbu kwa njia nyingine pale kupiga picha au kurekodi video si salama au hakuwezekani.
- Epuka masharti ya kiufundi yasiyo ya lazima au vifaa vya gharama kubwa.
- Heshimu jinsi watu wanavyochagua kuonyeshwa, wakiwemo watu wenye ulemavu.

Hatua ya kijamii yenye maana haipaswi kuachwa kamwe kwa sababu tu mtu hawezi kutoa picha au video za kiwango cha kitaalamu.

Jinsi ya kuwasilisha picha na video zako

Kwa kila hatua ya kijamii, tunapendekeza uwasilishe:

Picha 3–6	Ikiwezekana zionyeshe tatizo, shughuli na matokeo.
Video 1 fupi (hiari)	Takribani sekunde 30–60.
Maelezo mafupi	Tatizo lilikuwa nini? Ulifanya nini? Nini kilibadilika?
Mahali	Jamii yako au eneo kwa ujumla, bila kufichua anwani za makazi.
Ruhusa	Thibitisha kuwa una ridhaa inayohitajika kuwasilisha maudhui haya.

Wasilisha faili halisi pale inapowezekana, badala ya picha za skrini au nakala zilizobanwa sana.

Kama huwezi kupiga picha au kurekodi video kwa usalama, wasiliana na timu ya Action Challenge kuhusu njia nyingine za kuhifadhi kumbukumbu ya hatua yako.

Jinsi Amplified Access inavyoweza kutumia picha na video zako

Picha na video zilizowasilishwa zinaweza kuisaidia Amplified Access:

- Kuthibitisha na kuhifadhi kumbukumbu za hatua za kijamii.
- Kutambua juhudi za jamii zinazoshiriki.
- Kushiriki hadithi za mabadiliko yanayoongozwa na jamii.
- Kuonyesha matokeo na mafunzo yaliyopatikana.
- Kuhamasisha jamii nyingine kuchukua hatua.
- Kutoa taarifa kuhusu shughuli na matokeo ya Action Challenge.

Kuwasilisha maudhui hakutoi moja kwa moja ruhusa ya kuyatumia hadharani.

Amplified Access itaomba ruhusa inayofaa kabla ya kuchapisha maudhui yanayowatambulisha watu kwenye tovuti yake, mitandao ya kijamii, ripoti, mawasilisho au njia nyingine za mawasiliano ya umma.

Washiriki wanapaswa kuwasilisha tu maudhui waliyotengeneza wenyewe au walio na ruhusa ya kuyashiriki.

Jinsi tunavyolinda picha na video zilizowasilishwa

Amplified Access imejitolea kushughulikia kwa uwajibikaji picha, video na taarifa binafsi zilizowasilishwa. Tutafanya yafuatayo:

- Kukagua maudhui yaliyowasilishwa kuhusu faragha, usalama na ridhaa kabla ya kuyashiriki hadharani.
- Kuruhusu tu wanatimu walioidhinishwa na wakaguzi husika kufikia maudhui yaliyowasilishwa.
- Kuhifadhi maudhui yaliyowasilishwa kwa usalama na kuyaweka kwa muda unaohitajika tu kwa madhumuni halali ya mpango.
- Kuondoa taarifa zilizofichwa ndani ya faili (metadata) zinazoweza kumtambulisha mtu, ikiwemo mahali kamili, kabla ya kushiriki hadharani pale inapofaa.
- Kuepuka kuchapisha taarifa binafsi nyeti au maelezo yanayoweza kuwatambulisha watu na kuwaweka hatarini.

- Kuheshimu maombi ya kuondoa au kuacha kutumia maudhui yanayomtambulisha mtu, kwa kuzingatia wajibu wa kisheria na mipaka ya kiutendaji.
- Kupata ruhusa inayofaa kabla ya kushiriki maudhui yanayowatambulisha watu na washirika wa nje au vyombo vya habari.

Kwa maswali, wasiwasi kuhusu faragha, au maombi ya kuondoa maudhui, wasiliana nasi kwa hello@amplifiedaccess.org.

Orodha ya mwisho kabla ya kuwasilisha

Kabla ya kuwasilisha, thibitisha:

- ☑ Picha au video zangu zinaonyesha hatua halisi ya kijamii.
- ☑ Maudhui yanaeleza wazi kilichotokea na kilichobadilika.
- ☑ Watu wanaoweza kutambulika wamekubali kurekodiwa na kujumuishwa katika uwasilishaji huu.
- ☑ Nimechukua tahadhari zinazofaa kulinda watoto na watu walio hatarini.
- ☑ Hakuna taarifa binafsi nyeti au maelezo ya mahali yasiyo salama yanayofichuliwa.
- ☑ Maudhui ni ya heshima, ni ya kweli, na yanaonyesha hatua ilivyokuwa kwa usahihi.
- ☑ Nina ruhusa ya kuwasilisha maudhui haya.
- ☑ Ninaelewa kuwa kushiriki hadharani kunahitaji ruhusa tofauti.

KUMBUKA

Hatua yako ni muhimu kuliko ubora wa kamera yako.

Huhitaji vifaa vya kitaalamu, mwanga kamili, wala video iliyopambwa. Kilicho muhimu ni kuonyesha jamii yako ilifanya nini, nini kilibadilika, na wengine wanaweza kujifunza nini kutokana na uzoefu wako.